Chuka University
info@chuka.ac.ke | 020 231 0512 / 020 231 0518

# USE OF CHARACTERIZATION AS A STYLISTIC DEVICE IN KISWAHILI NOVEL: EXAMPLE FROM SIKU NJEMA AND KIDAGAA KIMEMWOZEA NOVELS-KEN WALIBORA.

***Allan Mugambi***

*Humanities department, Chuka University, P. O. Box 109-60400 Chuka. Email: a.mugambi@chuka.ac.ke*

**How to cite:**

Mugambi, A. (2022). Use of characterization as a stylistic device in Kiswahili novel: Example from siku njema and kidagaa kimemwozea Novels-Ken Walibora. In: Isutsa, D. K. (Ed.) *Proceedings of the 7th International Research Conference held in Chuka University from 3rd to 4th December 2020, Chuka, Kenya*, p.443-448

## ABSTRACT

Characterization is an important literary device that is used to highlight and explain the details of a character in the story. Characterization has to be gradual and in line with the progress of the story. Characterization can also be direct or indirect. Direct characterization is where the author takes a direct approach by building the character. He /she uses another character or a protagonist to tell the readers about the qualities of the character in question. In indirect characterization, the readers are left on their own to deduce on the traits of the character through observing their behaviors, talks, dressing or actions. Furthermore, well-defined characters will make the reader to identify with his or her attributes thus leaving an indelible mark on their minds. This paper interrogates the stylistic devices used by Ken Walibora in constructing and shaping his characters notably the protagonists and the antagonists in his stories. Ken walibora is a renown Kiswahili novelist with over 40 titles in his name. Some of his books have been used as class readers and tested during final secondary school examination in Kenya for a long time. His unique style of writing endeared him to many readers and contributed in popularizing his works beyond the borders of Kiswahili speakers. Thus this paper will use examples from his two novels *Siku Njema* and *Kidagaa Kimemwozea* authored in 1996 and 2012 respectively.

**Keywords:** Characterization, literary devices, protagonist, antagonist, novel

# USAWIRI WA WAHUSIKA KAMA MTINDO WA MWANDISHI KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI: MFANO KUTOKA RIWAYA YA SIKU NJEMA NA KIDAGAA KIMEMWOZEA-KEN WALIBORA.

***Allan Mugambi***

*Idara ya fani, Chuo Kikuu cha Chuka S.L.P 109-60400, Chuka. Barua pepe: a.mugambi@chuka.ac.ke*

**How to cite:**

Mugambi, A. (2021). Usawiri wa wahusika kama mtindo wa mwandishi katika riwaya ya Kiswahili: mfano kutoka riwaya ya siku njema na kidagaa kimemwozea-Ken Walibora. In: Isutsa, D.K. (Ed.) *Proceedings of the 7th International Research Conference held in Chuka University from 3rd to 4th December2020, Chuka, Kenya*, p.443-448

## IKISIRI

Usawiri wa wahusika ni kiunzi muhimu katika kufanikisha kazi yoyote ya sanaa. Mwandishi huwatumia wahusika kama kipasa sauti chake ili kujenga uhusiano na wasomaji sawia na kuwasilisha maudhui yake kwa hadhira. Aidha, wahusika mahiri huvutia wasomaji kiasi kwamba mawazo ya mwandishi yatapitishwa kwa urahisi na kupokelewa bila pingamizi. Ken Walibora ni mwandishi maarufu katika fasihi ya Kiswahili ambaye ameandika zaidi ya vitabu 40 maishani mwake. Baadhi ya vitabu vyake vimetumiwa kwa muda mrefu katika ufunzaji na utahini wa mtihani wa mwisho katika shule za upili nchini Kenya. Upekee wa mwandishi huyu unajitokeza katika mbinu zake za utunzi pamoja na maudhui yanayopokelewa na kueleweka na wengi. Usawiri wake wa wahusika umewafanya vijana wengi

kuchangamkia vitabu vyake na kuvikumbuka kwa muda mrefu hata baada ya kumaliza mfumo wao wa masomo. Makala hii inalenga kuchunguza mbinu za usawiri wa wahusika zinazompatia umaarufu katika utunzi wake. Wahusika katika riwaya za Siku Njema na Kidagaa Kimemwozea watachunguzwa ili kufanikisha lengo hili.

Maneno muhimu: Uhusika, mtindo, hadhira, riwaya, usawiri

## UTANGULIZI

### Usuli Wa Mada

Wahusika ni viumbe walioumbwa na mwandishi ili kuendeleza dhima ya sanaa. Waandishi huwaumba viumbe vyao kutokana na vipengele vya maisha ya binadamu wa kawaida. Aidha wanakuza baadhi ya sifa na kupuuza zingine na baadaye kuibua viumbe wanaoshabii uhalisia wa ulimwengu halisi tunamoishi. Ingawa baadhi ya wahusika ni wanyama, wadudu na viumbe visivyo hai, wale wahusika binadamu wamefanikiwa zaidi katika fasihi. Lodge 1992 anahoji kuwa uhusika katika kazi za sanaa, huwa ni kipengele kigumu kuwasilisha. Anasema kuwa kufanikisha usawiri wa wahusika hutawaliwa na mambo mengi katika fasihi kama vile, ploti, mbinu ya usimulizi, mandhari na mtindo wa mwandishi. Kutokana na mtagusano huu wa vipengele mbalimbali ndipo wahusika huibuka, huzungumza na kuingiliana na wengine katika mandhari ya sanaa. Akigusia suala la uhusika katika sanaa Wamitila (2002), anasema kuwa usawiri wa wahusika, wasifu wao, tabia zao, lugha yao, itikadi, vionjo na hata mitazamo yao huathiriwa kwa kiasi kikubwa na dhamira ya kazi fulani ya kifasihi.

Fasihi huwa na aina mbalimbali ya wahusika. Kuna wahusika duara ambao hubadilika mara kwa mara kulingana na hali wanayopitia. Kuna wahusika bapa pia ambao hawabadiliki kamwe. Hawa hutambulika kwa urahisi na athari zao huwa wazi. Wahusika pia wanaweza kugawanywa kuwa wahusika wakuu au wale wasaidizi kutokana na mchango wao kwa kazi ya sanaa. Wahusika wakuu hushirikishwa katika hadithi nzima na hutamba katika kila sehemu. Wahusika wasaidizi hutumika kwa muda tu kulingana na malengo ya mwandishi, kisha wanatoweka baada ya kutimiza lengo lao. Ubunifu wa wahusika ili waweze kuvutia wasomaji ni kazi inayohitaji ustadi na uangalifu mkubwa. Sharti wahusika waaminike na wawe na msukumo bayana kwa yale wanayotenda. Msomaji anafaa kujinasibisha na mhusika fulani ikiwa amebuniwa vizuri bure sivyo, kazi ya sanaa itakuwa na udhaifu.

Kazi za sanaa zilizofaulu huwa na wahusika waliobuniwa vizuri. Waandishi hata hivyo wana uhuru wa kuwabuni wahusika wao jinsi wanavyotaka bora waaminike na pia waweze kukuza lengo lao. Mwandishi kama vile Mohammed S. Mohammed aliyeandika riwaya mashuhuri ya *nyota ya rehema* aliwatumia wahusika makahaba katika kuwasilisha maudhui yake. Jinsi wahusika wake wanavyozungumza, kutenda na hata kuvalia, humuacha msomaji na taswira kamili ya shughuli zao za kutafuta riziki. Saidi A. Mohammed ni mwandishi mwingine mashuhuri katika fasihi ya Kiswahili. Mohammd ameandika riwaya kadha kama vile *utengano*, *dunia mti mkavu* na *asali chungu*. Ametumia mitindo kadha kusawiri wahusika wake.

Alipoandika riwaya zake alitumia wahusika wa kihalisia wenye sifa zinazofanana na binadamu wa kawaida. Mtindo wake hata hivyo ulibadilika alipotunga riwaya ya *babu alipofufuka* inayoongozwa na mtazamo wa kihalisia ajabu. Amewachora wahusika wa kiajabu ajabu katika riwaya hii, ambao wanatenda matendo yasiowezekana kutendwa na watu wa kawaida. Mhusika mkuu kama vile babu anafanana na mzuka. Mohammed alifaulu katika kuonyesha uhusiano ulioko kati ya ulimwengu halisi na ule wa kijonzi. Ametumia mbinu kadha kama mandhari na usimulizi ili kutuchorea wahusika wake wasio wa kawaida. Ubunifu wake unamuacha msomaji na taharuki ya kutaka kujua yanakayojiri na jinsi wahusika watakabiliana na hali mbalimbali, suala linalochangia kuendeleza maudhui yake.

Mifano iliyotajwa hapo juu inaonyesha bayana kuhusu umuhimu wa uhusika katika kazi za sanaa. Wahusika ni kama vipasa sauti vya waandishi. Usawiri bora wa wahusika ni stadi inayokuzwa na kuimarishwa katika tajriba ya uandishi. Masuala kama haya yalichochea makala hii ili kuchunguza kiini cha umaarufu wa riwaya zilizoandikwa na Ken Walibora. Kuna vipengele vingi vya fani ambavyo vingechunguzwa katika kazi hii lakini kipengele cha wahusika kilichaguliwa maksudi. Sababu ni kuwa wahusika huwakilisha wanajamii wanaorejelewa na mwandishi na hudhihirisha kwa njia ya wazi zaidi maudhui yaliyokusudiwa katika kazi ya sanaa. Uteuzi wa mifano kutoka riwaya zilizoandikwa na Ken Walibora pia ulikuwa wa kimaksudi. Kuna upekee wa aina fulani katika usawiri wa wahusika kwenye kazi za Ken Walibora. Ingawa mwandishi huyu amefanikiwa kuandika zaidi ya vitabu 40, ametumia wahusika vijana kwa wingi katika kazi zake. Wahusika hawa wanahusishwa katika mambo mengi na hasa safari wanazofunga. Motifu ya safari ni dira muhimu inayoongoza kazi nyingi za Walibora. Kutokana na safari za wahusika, mwandishi anapata fursa ya kuwajenga na kuwakuza na kuweka wazi sifa za wahusika mbalimbali. Safari hizi pia zinachangia mgao wa wakati ulio na mantiki katika kujenga hulka ya wahusika. Suala hili linamfanya msomaji awe mshiriki wa mwandishi hasa katika kukisia yale yanayoweza kutendwa ama kukumbana na mhusika fulani. Kwa misingi hii Ken amefaulu kukuza wahusika wake kwa njia ya kipekee. Aidha, tajriba za mwandishi huathiri mbinu zake za utunzi pamoja na usawiri wake wa wahusika na maudhui anayowasilisha. Pana haja ya kuangazia maisha ya Ken Walibora kwa muhtasari ili kutoa mwanga zaidi kuhusu mada inayoshughulikiwa.

**Maisha Ya Ken Walibora**

Ken Walibora alikuwa mwandishi mashuhuri wa fasihi ya Kiswahili ambaye alifanikiwa kuandika zaidi ya vitabu 40 kabla ya kuaga dunia. Kennedy Atanasi Waliahula alizaliwa mnamo tarehe 6, Januari mwaka wa 1965. Alijiunga na shule ya msingi ya St. Joseph mjini Kitale kabla ya kwenda katika shule ya upili ya Olkejuado na Koelel mtawalia. Baada ya masomo yake katika shule ya upili alijiunga na chuo kikuu cha Nairobi kusomea shahada ya kwanza ambapo alibobea katika somo la fasihi. Baadaye alijiunga na chuo kikuu cha Ohio nchini Marekani ambako alisomea shahada ya uzamifu na kuandika tasnifu yake kuhusu fasihi ya gerezani. Ken alikuwa mwanahabari, mwalimu, msomi na mwandishi. Ken alifunza katika chuo kikuu cha Madison Wisconsin Marekani kwa muda mrefu.

Baadaye alijiunga na chuo kikuu cha Riara nchini Kenya ambako aliendelea kufundisha na kuandika pamoja na shughuli zingine za kitaaluma. Matundura (2020), anasema kuwa Ken alifanikiwa kutunga na kuchapisha tungo nyingi katika mapana na marefu ya tanzu zote za fasihi. Mwanataaluma huyu alipata umaarufu wa kimataifa kutokana na mtindo wake wa usanii hasa katika riwaya ya Kiswahili. Kutokana na ustadi wake wa utunzi, kazi zake zimepokelewa na wasomi kote ulimwenguni na zinaendelea kusomwa. Baadhi ya riwaya zake ni kama vile *siku njema*, *ndoto ya almasi*, *ndoto ya marekani*, *kufa kuzikana*, na *kidagaa kimemwozea*. Ameandika tamthilia za *mbaya wetu* na *kisasi hapana*. Katika ulingo wa hadithi fupi aliandika *maskini milionea na hadithi zingine* pamoja na *damu nyeusi na hadithi zingine* miongoni mwa kazi nyingi.

Walibora alikuwa na kipawa cha kusimulia matukio na kuyapanga kwa utaratibu uliosisimua msomaji na kumucha na shauku ya kusoma zaidi. Njogu (2020), anasema kuwa umilisi wa Walibora katika lugha ya Kiswahili na maisha ya watu wa kawaida ulimpa nyenzo muhimu za utunzi. Aliweza kutumia jazanda na vipengele vingine vya fani kwa kiwango kisicho cha kawaida. Nchini Kenya, baadhi ya vitabu vyake vimetumiwa katika kufunzia fasihi ya Kiswahili hasa riwaya na kutahiniwa katika mitihani ya mwisho ya kidato cha nne. Riwaya yake ya *siku njema* alioandika katika mwaka wa 1996 ilifungua ukurasa mpya katika fasihi ya Kiswahili. Matundura (2020), anasema kuwa riwaya hii ilikuwa miongoni kwa kazi zilizoipatia fasihi ya Kiswahili msukumo na nguvu mpya.

Walibora amefanikiwa katika kutumia mbinu mbalimbali za kisanaa. Usawiri wake wa wahusika ni suala linalohitaji kuchunguzwa kwa sababu waliosoma vitabu vyake huwapokea wahusika wake barabara na kuwakumbuka hata baada ya miaka mingi ya masomo. Mapitio yake ya maisha, tajriba yake pamoja na utafiti wake wa jamii ni baadhi ya mambo yaliyompatia nafasi adhimu ya kujenga wahusika maarufu waliotajika na wenye sifa za kuaminika katika kazi zake. Suala hili linadhihirisha bayana kwamba mwandishi wa fasihi haandiki katika ombwe tupu bali huchota maudhui yake katika jamii anamoishi, hasa yale aliyoyaona ama kuyasikia. Walibora aliaga dunia mnamo tarehe kumi mwezi wa Aprili 2020 akiwa na umri wa miaka 55.

**Wahusika Katika Riwaya Za Siku Njema Na Kidagaa Kimemwozea**
Riwaya za *siku njema* na *kidagaa kimemwozea* ziliandikwa na Ken walibora katika mwaka wa 1996, na 2012 mtawalia. Riwaya hizi zimetumia motifu ya safari kama mbinu ya utunzi. Mbinu hii huhusisha safari maalum inayofanywa na mhusika mkuu katika hali ya kutafuta ukweli fulani unaohusiana na maisha yake na maisha ya jamii kwa jumla. Wahusika wakuu wanajisaka na kujitafuta na hatimaye hufanikiwa kupata jawabu wanalosaka. Mara nyingi, wahusika hupata ufafanuzi ulio kinyume na yale waliokuwa wanasaka na hujifunza unyenyekevu au hata ujasiri katika msako wao. Ingawa mbinu hii ilitumika tangu enzi za kale, Walibora ameitumia kwa ufanisi mkubwa hasa katika usawiri wake wa wahusika. Riwaya za *siku njema* na *kidagaa kimemwozea* ni mifano madhubuti ya kudhihirisha ukweli huu. Riwaya ya *siku njema* ina mhusika mkuu ambaye kwa jina ni Kongowea Mswahili.

Mhusika huyu alizaliwa mjini Tanga katika nchi ya Tanzania. Alipozaliwa baba yake hakujulikana na aliitwa mwana haramu. Kongowea hata hivyo, alikuwa na kipawa cha uandishi. Kutokana na ushindi wake katika mashindano ya uandishi mkoani Tanga, wanafunzi wenzake wanampa jina la lakabu Kongowea Mswahili. Kutokana na madhila haya ya kuitwa mwana haramu Kongowea anafanya msako mkali wa kumtafuta babake mzazi. Msako huu unampeleka hadi nchini jirani ya Kenya. Anakumbana na mengi katika safari yake yakiwemo wahusika wengine wa hulka tofauti. Safari yake imejaa dhiki, taharuki na masaibu ya aina nyingi. Baadaye alifanikiwa kumpata babake aliyejulikana kama Juma Mukosi ambaye alitumia lakabu katika maandishi yake yaani Amuj Isokum. Msako huu unaweza kulinganishwa na hali halisi ya wanajamii wanaojaribu mengi ili kuboresha maisha yao pamoja na kutafuta haki. Mengi hutokea katika safari hii ya maisha ambapo wengine hukata tamaa na wengine huendelea kupambana. Motif ya safari inatoa fursa muhimu ya kukuza na kujenga wahusika wa kuaminika. Kutokana na mandhari wanayopitia, wahusika wengine wanaokumbana nao pamoja na changamoto mbalimbali sifa mbalimbali za wahusikahuweza kudhihirika.

Wahusika katika riwaya ya *kidagaa kimemwozea* pia wako safarini ya kusaka haki. Kupitia msako huu, tunapata hali halisi ya wanyonge ambao wananyanyaswa kwa kila njia na watawala na mabwanyenye. Hata hivyo, wanyonge wanaamua kujikomboa na kufanya mapinduzi yanayoletwa na vijana. Amani na Imani ambao ndio wahusika walio katika mstari wa mbele wa kuleta mabadiliko wamesawiriwa miongoni mwa wahusika wakuu. Vijana hawa wanavunja miiko na kuendeleza mapinduzi ya kila aina. Wana ujasiri, bidii, utu, msimamo dhabiti, na werevu. Wanapambana na wahusika wengine ambao ni mahasidi wao kama vile Mtemi Nasaba Bora na Majisifu Majimarefu. Kuna wahusika wasaidizi mbalimbali waliosawiriwa na ambao pia wanachangia dhamira kuu ya riwaya hii kama vile, Dora, Zuhura, Dj Gadafi na Fao.

**Mbinu Za Usawiri Wa Wahusika Katika Riwaya Teule**
Walibora ametumia njia kadhaa katika kuwasawiri wahusika wake. Anaibua wahusika moja kwa moja na kwa lugha rahisi inayomfanya msomaji kuona kama alimfahamu mhusika tangu mwanzo. Ametumia usimulizi wa nafsi ya kwanza katika riwaya ya *siku njema*. Usimulizi wa aina hii hutumika zaidi katika riwaya za tawasifu. Walibora alipoutumia katika riwaya hii, msomaji alihisi kana kwamba mwandishi mwenyewe alikuwa anasimulia maisha

yake binafsi. Mtindo huu ulimfanya msomaji kuamini masimulio haya zaidi na kuyamakinikia. Ukweli ni kwamba kisa chenyewe kiikuwa cha kubuni wala hakikuhusikana na maisha ya mwandishi. Mkabala huu vilevile unamfanya msomaji kujifananisha na nguli katika hadithi inayosimuliwa. Kuna uhusiano unaochipuka kati ya mhusika wa aina hii na msomaji. Hali hii inamfanya msomaji kupenda mhusika anayerejelewa katika mtazamo huu. Vijana wengi waliosoma riwaya ya *siku njema* wamekiri kwamba waliathiriwa pakubwa na mhusika mkuu Kongowea Mswahili. Usomaji wa kazi hii kwao ulikuwa kama tafakuri ya moyo ambapo walianza kudadisi upya mwelekeo wa maisha yao. Ingawa mhusika Kongowea Mswahili alikuwa kiumbe cha kubuni, alionekana mwanadamu halisi kwa momaji.

Mbinu ya kimaelezo pia imetumika kwa ufanisi mkubwa. Katika mbinu hii, mwandishi huelezea sifa za mhusika fulani na kujenga taswira dhabiti kumhusu. Mbinu hii humpatia mwandishi uhuru wa kudhihirisha chuki au mapenzi kwa mhusika anayerejerewa. Mwandishi huweza kutoa maelezo anayotaka kuhusu wahusika mbalimbali. Hata hivyo, mbinu hii haimpi msomaji nafasi ya kuchunguza tabia za mhusika fulani suala linaloweza kuwa changamoto. Walibora alifidia upungufu huu kwa kutumia mazungumzo ya wahusika wenyewe kwa wenyewe ili kutoa sifa zaidi.

Mfano mhusika Majisifu Majimarefu katika riwaya ya *Kidagaa kimemwozea* anapoenda kutoa hotuba kuhusu kitabu chake katika chuo kikuu cha Mkokotoni, anaulizwa maswali anayoshindwa kujibu…(uk. 124). Maswali anayoulizwa yanatupa sifa zake kadhaa; kwamba hakuwa mwandishi wa mswada huu na pia alikuwa haufahamu wala kuuelewa mswada huu, jambo linalomsawiri kama mtu mwenye akili ndogo. Maneno ya Majisifu Majimarefu katika kujitetea kwake yanatilia nguvu kupungukiwa kwake kwa akili na kukosa falsafa. Anawasifia wafalme madikteta wa kiafrika kama Amin Dada wa Uganda na Bokasa wa Jamhuri ya Afrika ya Kati na kushangaza halaiki katika ukumbi mzima. Mambo haya yanadhihirisha sifa zake hasi ambazo mwandishi alikuwa amemwekea na kuathiri mtazamo wa msomaji kumhusu kwa kiwango kikubwa.

Walibora pia amefaulu kutumia mbinu ya ulinganuo katika kuwasawiri wahusika wake. Mbinu hii inalinganisha wahusika wawili kwa njia ya kinyume. Baadhi ya wahusika wana tabia ambazo zinapingana. Tunaona Mtemi Nasaba Bora katika riwaya ya *kidagaa kimemwozea* akiwa mtu bidhuli. Anawanyanyasa watu kwa kila namna ikiwa ni pamoja na kuwanyang’anya mashamba yao, mabinti, wake na hata mali. Anatumia askari na jela kuwatishia raia katika janibu ya Sokomoko. Kinyume na mhusika huyu tunamwona Amani ambaye ni mtetezi wa haki za wanyonge. Ana utu na mvumilivu asiyetaka kulipisha kisasi. Amani anasema’ mimi sina ngoa na yeyote, ujaponitenda ubaya sina chuki nawe… (uk. 147)’ Kauli hii inaonyesha moyo wa kusamehe licha ya kutetea haki. Taswira ya wahusika hawa wawili waliosawiriwa kwa sifa zilizokinzana inanata akili ya msomaji na kufanikisha ploti nzima ya riwaya.

Mwandishi pia alitumia mbinu ya majazi kwa wingi. Majazi ni mbinu ya sanaa inayohusisha majina ya wahusika au mahali fulani na sifa au tabia zao. Majina ya wahusika katika mbinu hii huakisi sifa, wasifu, itikadi, mandhari na hata matamanio yao. Wahusika kama vile Amani na Imani wamesawiriwa kwa kutumia mbinu hii. Amani kwa mujibu wa Tuki 1988 ni hali ya kuwa salama bila ghasia au fujo. Mhusika Amani anasawiriwa kama mtu aliye na utulivu mwenye utu na asiyependa fujo wala udanganyifu. Imani kwa upande mwingine ni itikadi inayomfanya mtu kuwa na mkabala fulani wa maisha. Mtu mwenye imani huwa na maono fulani ya moyo kuhusu jambo au kitu. Mhusika Imani katika riwaya hii ya *Kidagaa kimemwozea* anakuwa wa kwanza kuyanywa maji ya mto Kiberenge kinyume na itikadi za jamii yao. Watu wanashangaa kwamba hakuaga dunia kinyume na ilivyoaminika.

Mhusika huyu aliamini kwamba jambo ambalo lilikuwa haramu lingeweza kuhalalishwa. Jina lake Imani linaendanisha na sifa zake katika riwaya hii. Mhusika Mtemi Nasaba Bora, anawakandamiza wananchi na kuwatawala kwa ufito wa chuma. Anawanyang’anya mashamba, wake mabinti na hata mali zao. Wananchi wanamwogopa na hawangesema chochote cha kumpinga. Jina Mtemi lilitumiwa na jamii ya wanyamwezi kurejelea watawala wao waliokuwa wakali sana. Waliweza kuwashambulia maadui zao bila huruma. Jina hili linatumika kimajazi hapa kuonyesha udikteta ulioendelezwa na mfalme huyu katika nchi ya Sokomoko. Mfano wa mwisho kudhihirisha mbinu ya majazi ni jina la mwalimu majisifu Majimarefu lililotumika kimajazi kwa sababu anaiba mswada wa wengine na kujisifu alivyoandika kitabu. Anashindwa kutetea kazi yake alipoenda kutoa hotuba katika chuo kikuu cha Mkokotoni, jambo linalomfedhehesha mno.

Mbinu ya kuwatumia wahusika wengine ili kufafanua sifa za wenzao imetumiwa kwa mapana na Walibora. Wahusika huelezea matendo, mienendo na sifa za wenzao kwa njia ya kawaida tu kama inavyofanywa katika mazungumzo. Kutokana na mawasiliano haya tunaweza kupata sifa mbalimbali za wahusika wanaorejelewa.

Maneno haya yanatufichulia matendo yaliyotendwa na mhusika na hata kumuumbua. Katika riwaya ya *kidagaa kimemwozea* tunaona Bibi kizee analalamikia kule kulazimishwa kuhudhulia sherehe na Mtemi Nasaba Bora pale Sokomoko. Weye aliyekuwa mwendawazimu anasema kuwa Memi amewapokonya mashamba, mali, mabinti na hata wake zao. Bi Rahma katika riwaya ya *siku njema* anasema mengi kuhusu marehemu Zainabu; kwamba alikuwa mkarimu, muungwana hakupenda ugomvi wala kumuudhi mtu… (uk. 29). Kupitia kwa maneno ya wahusika hawa tunapata kupata sifa za wahusika wenzao.

Maneno ya mhusika binafsi na mienendo yake ni mbinu nyingine iliyotumiwa na mwandishi Walibora katika kufanikisha usawiri wa wahusika wake. Wale wahusika katili kama vile Selemani na wenzake wanatumia maneno ya vitisho na lugha kali katika riwaya ya *siku njema*. Tunaona Mtemi Nasaba Bora katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* akiamrisha kushikwa kwa Amani na Imani kwa vizingizio tu. Askari wanatumia lugha isiyokuwa na adabu na kuwatukana watu, jambo ambalo ni la kawaida kwa askari. Mtemi Nasaba Bora anatukana hata bibi yake bila kujali. Mienendo ya Mtemi yanatufichulia mengi kuhusu tabia zake. Alikuwa mwepesi wa hasira na mtu mwenye tabia za ufuska. Licha ya kuwa na bibi kwa jina Zuhura, anaweka kimada kwa jina Lowela Maozi na kuendeleza mahusiano ya kimapenzi nje ya ndoa yake…uk. 106.

Mandhari pia ni mbinu iliyotumika kujenga baadhi ya wahusika katika kazi zinazorejewa. Sababu ni kuwa kila kitendo cha fasihi hufanyika katika mandhari maalum. Mandhari hutueleza kuhusu wapi na ni lini kitendo fulani kilitendeka. Kwa misingi hii, tunaweza kufahamu hisia za wahusika, hasira, kero tamaa na utu ama unyama. Mfano tunamwona Mtemi Nasaba Bora katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* akimkuta Amani na bibi yake Zuhura chumbani mwake katika hali ya kutatanisha. Jambo hili linamghadhabisha na anapandwa na mori haraka.

Anakimbilia bunduki yake hata bila kudadisi sababu za yale yaliyokuwa yakitendeka chumbani mwake. Anampiga Amani kwa mtutu wa bunduki kwa nguvu zake zote na kumwangusha chini…(uk. 132). Hiki ni kitendo cha unyama kinachosababishwa na hasira ya bwana Mtemi. Uwanjani wa Nasaba Bora tunakuta wahusika wengine askari ambao wanalinda Mtemi, Mhusika Weye alikuwa ni mwenda wazimu na anachangia kutwambia mengi ambayo watu razini hawangeyasema kwa hofu ya kuwekwa gerezani. Mandhari ya uwanja yanachangia kusawiri sifa za wahusika hawa kwa sababu wahusika kama hawa hupatikana katika sherehe katika hali ya kawaida.

Waliboraaliweza kuwabuni wahusika wake pia kupitia ucheshi pamoja na mbinu zingine za fani kama kinaya, chuku, jazanda na tashbihi. Baadhi ya wahusika wanatenda matendo tunayoona kama si rahisi kutokea katika hali ya kawaida. Hata hivyo yanawasilishwa kwa urahisi kana kwamba yalitokea hakika. Tunaona kwa mfano mhusika Amani akishawishiwa na bibi ya Mtemi Nasaba Bora kuingia chumbani mwake wakati wa usiku. Bi Zuhura amevalia vasi la kutatanisha lakini Amani haonekani kujali. Amani anakubali kuingia chumbani cha kulala cha Mtemi Nasaba Bora bila kutafakari kuhusu agizo hili ambalo halikuwa la kawaida. Bi Zuhura na Amani hatimaye wanavumaniwa pale ndani na Mtemi na kushambuliwa vikali… *Kidagaa Kimemwazea* (uk. 131).

Hili si jambo la kawaida kutokea ingawa mwandishi analieleza kwa ushawishi na kumfanya msomaji aliamini. Ilikuwa kinaya kwa Mtemi kutumia Kiingereza kuzungumza na raia ingawa hawakung'amua chochote. Mbinu hii inatoa sifa za wahusika hawa na kuendelea kuonyesha tabia zao… *Kidagaa kimemwozea* …(uk.70). Baada ya kifo cha Rashid ambacho kilitokea siku tatu kabla ya arusi, tunamwona mpenzi wake Zawadi akimwomba Kongowea kumuoa katika riwaya ya *Siku Njema*. Anafanya hivi licha ya kujua kuwa alikuwa mvulana wa miaka kumi na sita pekee. Ombi kama hili si la kawaida kulingana na mila na desturi za jamii nyingi hasa barani Afrika. Mwandishi hata hivyo analiwasilisha kwa njia ya moja kwa moja ili kujenga sifa za mhusika wake mkuu Kongowea Mswahili… (uk.97).

**HITIMISHO**

Makala hii imedhihirisha bayana kwamba mwandishi Ken Walibora alifanikiwa katika kusawiri wahusika wake kwa kiwango kikubwa. Ingawa baadhi ya mbinu alizotumia ni zile za kawaida, anafidia kwa kuunganisha na mtindo wake wa uandishi pamoja na vipengele vya fani kiasi kwamba mbinu zake zinakaa kama ni mpya kabisa. Makala hii pia imedhihirisha kuwa mwandishi ametumia mbinu kadhaa za usawiri wa wahusika ili kufanikisha kazi zake za uandishi. Baadhi ya mbinu alizotumia ni pamoja na maelezo, majazi, matendo ya wahusika, maneno ya wahusika wengine kuhusu wenzao na mbinu ya mlinganuo. Aidha, mwandishi ametumia motifu ya safari katika kupambanua mawazo yake. Kupitia mbinu hii, Walibora anafanikiwa kukuza wahusika wake kwa kina na kwa njia ya kuaminika.

Aliweza kuonyesha wahusika wake katika mazingira mbalimbali na tabia walizofanya katika hali hizo kupitia safari zao. Tunaona mabadiliko ya wahusika kutokana na yale waliyopitia na kuona. Yaliyosemwa na kufanywa na wahusika hawa yalichangia katika kufanikisha dhamira kuu ya riwaya teule. Safari walizofunga pamoja na sehemu walizopitia zilitoa nafasi ya kuwakuza na kuwajenga wahusika wanaorejelewa na mwandishi. Mtindo wa Walibora wa uandishi na usawiri wa wahusika ni sifa muhimu zinazomtambulisha mwandishi huyu na kuchangia kupokelewa kwa riwaya zake na wasomaji.

**MAREJELEO**


Lodge, D. The Art of Fiction, retrieved on 20/12/2020 from. www.pdfdrive.com/lodge-the-art-of-fiction-e18828274.html

Matundura B. ( 2020. Buriani mwanasafu mwenza Ken Walibora. Ilipakuliwa tarehe 22 Disemba 2020 kutoka www.taifaleo.nation.co.ke

Njogu, K. (2020). Careless Driving Drops the Curtain on One of Africa's Best Storytelling, kutoka www.standardmedia.co.ke

Njogu K. Na Chimerah (1999). *Ufundishaji Wa Fasihi: Nadharia Na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Tuki (1988). *Kamusi sanifu ya Kiswahili*, Oxford University Press, Chuo kikuu cha Dar-es-salaam, Dar es Salaam.

Walibora, K. (2012). *Kidagaa Kimemwozea*. Nairobi: Spotlight

Walibora, K. (1996). *Siku Njema* Nairobi: Longhorn

Wamitila, K.W (2002). *Uhakiki wa Fasihi Msingi na Vipengele Vyake,* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.


**********